# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

# MUHTASARI WA RASIMU YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

## 1.0 UTANGULIZI

***Ndugu Mwenyekiti,***

Naomba kuchukua fursa hii kuwasilisha Muhtasari wa Rasimu ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha **2017/2018** ambayo imejadiliwa na kutolewa mapendekezo na Sekretarieti ya Mkoa, Kamati za Kudumu za Halmashauri, Baraza la Wafanyakazi na Baraza la Madiwani.

Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2017/2018** umeandaliwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka **2025**.
(ii) Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka **2015**.
(iii) Mwongozo wa uandaaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka wa fedha **2017/2018** uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.
(iv) Vipaumbele vya serikali ya awamu ya tano.
(v) Uzoefu wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha **2015/2016** na **2016/2017** hadi Desemba **2016**.
(vi) Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG)
(vii) Maelekezo ya Sera mbalimbali za Ki-sekta
(viii) Vipaumbele vya wananchi kutoka ngazi za kata na mitaa.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 NA 2016/2017

### 2.1 Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016

***Ndugu Mwenyekiti,***

Katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha **2015/2016,** Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya **Tsh.28,239,256,450.58** kama zinavyoonekana katika jedwali hapo chini.

| NA. | CHANZO | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA POKELEWA | ASILIMIA YA MAPOKEZI | MATUMIZI HALISI | ASILIMIA YA MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FEDHA ZILIZOVUKA MWAKA 2014/2015 | 1,194,030,353.07 | 1,194,030,353.07 | 100 | 1,162,851,906.26 | 97.39 |
| 2 | MAPATO YA NDANI | 2,145,947,100.00 | 1,752,861,447.39 | 81.68 | 1,261,721,699.75 | 58.80 |
| 3 | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | 2,655,794,001.30 | 2,056,728,500.00 | 77.44 | 2,295,849,928.23 | 80.99 |
| 4 | MISHAHARA | 18,232,905,300.00 | 17,278,173,033.50 | 94.78 | 17,281,174,033.13 | 94.78 |
| 5 | FEDHA ZA MIRADI | 4,010,579,696.21 | 5,315,162,514.17 | 132.43 | 4,101,326,448.38 | 102.26 |
| | **JUMLA** | **28,239,256,450.58** | **27,596,955,848.13** | **97.73** | **26,102,924,015.75** | **92.43** |

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha **2015/2016** pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kufikia asilimia **82** kutoka asilimia **62.5** kwa mwaka wa fedha **2014/2015**.

(ii) Upungufu wa madawati katika shule za msingi na sekondari umemalizika.

(iii) Kiwango cha ufaulu kwenye mtihani wa darasa la VII kiliongezeka kutoka asilimia **56.03** kwa mwaka wa fedha **2014/2015** hadi asilimia **76.95** kwa mwaka wa fedha **2015/2016**.

(iv) Kiwango cha ufaulu mtihani wa kidato cha II kiliongezeka kutoka asilimia **83.8** kwa mwaka wa fedha **2014/2015** hadi asilimia **88.5** kwa mwaka wa fedha **2015/2016**.

(v) Miundombinu ya shule za msingi na sekondari iliongezeka.

(vi) Vifo vya mama wajawazito vilipungua kutoka **217/100,000** hadi **204/100,000**.

(vii) Kiwango cha malaria kilipungua kutoka asilimia **49** hadi asilimia **27**.

(viii) Urefu wa barabara za lami umeongezeka kutoka km **9.23** hadi km **11.61**.

(ix) Barabara zote zinapitika baada ya kuboreshwa kwa kiwango cha changarawe.

(x) Kukamilisha mpango wa matumizi bora ya ardhi (General Planning Scheme).

## 2.2 Utekelezaji wa bajeti ya 2016/2017 hadi kufikia desemba, 2016

**Ndugu Mwenyekiti,**

Katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha **2016/2017**, Halmashauri iiidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs. 32,676,659,332.02** kama zinavyoonekana katika jedwali hapo chini.

| NA. | CHANZO | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA POKELEWA | ASILIMIA YA MAPOKEZI | MATUMIZI HALISI | ASILIMIA YA MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FEDHA ZILIZOVUKA MWAKA 2015/2016 | 1,494,031,832.42 | 1,494,031,832.42 | 100 | 1,162,851,906.26 | 77.83 |
| 2 | MAPATO YA NDANI | 1,833,390,000.00 | 897,384,217.08 | 48.95 | 773,772,333.00 | 42.20 |
| 3 | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | 2,556,766,000.00 | 1,123,772,251.00 | 43.95 | 1,261,721,669.75 | 49.35 |
| 4 | MISHAHARA | 17,733,133,000.00 | 8,246,582,422.79 | 46.50 | 8,246,582,422.79 | 46.50 |
| 5 | FEDHA ZA MIRADI | 9,059,338,499.00 | 3,976,852,874.33 | 43.90 | 1,610,361,665.37 | 17.78 |
| | **JUMLA** | **32,676,659,332.02** | **15,853,880,597.62** | **48.16** | **12,927,461,868.79** | **39.56** |

***Ndugu Mwenyekiti,***

Kwa ujumla hali ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa mwaka **2016/2017** sio ya kuridhisha. Halmashauri katika mwaka huu wa fedha **2016/2017** haijapokea fedha kutoka serikali kuu kwa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokusudiwa kutekelezwa kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara, programu ya uboreshaji miji (ULGSP) na ruzuku ya maendeleo (LGDG). Hata hivyo Halmashauri imeweza kutekeleza miradi michache kwa kutumia fedha ambazo tayari zimepokelewa.

Aidha Halmashauri imetekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani yenye jumla ya **Tsh. 221,077,950/=** kama ifuatavyo:-

1. Utengenezaji wa madawati kwa ajili ya shule za msingi na sekondari kwa gharama ya **Tsh. 70,168,950/=.**
2. Kuandaa wasifu wa mkoa na Halmashauri **Tsh**. **19,909,000/=.**
3. Kulipa deni la mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa **Tsh. 30,000,000/=.**
4. Mchango wa Halmashauri kwenye Mfuko wa Maendeleo ya wanawake na vijana **Tsh. 60,000,000/=.**
5. Mchango wa **20%** za kuwezesha miradi ya Mtaa na Kata ni **Tsh. 21,000,000/=.**

6. Ukarabati wa jengo la Utawala na vyoo Soko kuu **Tsh. 20,000,000/=.**

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI**

(i) Kuchelewa kutolewa au kutotolewa kabisa kwa fedha toka Serikali kuu.
(ii) Kuchelewa kutekelezwa kwa miradi ya maendeleo kutokana na mchakato mrefu wa manunuzi hususani programu ya uboreshaji wa miji (ULGSP).
(iii) Baadhi ya wananchi katika baadhi ya maeneo kutoshiriki kikamilifu katika kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohitaji uchangiaji wa nguvu za wananchi.
(iv) Kutorejeshwa kwa asilimia 30 ya kodi ya ardhi.

**MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

(i) Kubaini na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza wigo wa kukusanya mapato ili kupunguza utegemezi kutoka serikal ikuu.
(ii) Kupanua uwezo waHalmashauri kukusanya na kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya ki-elektroniki (LGRCIS).
(iii) Kuendelea kuwahimiza wananchi kupitia mikutano mbalimbali ili wachangie shughuli za maendeleo.
(iv) Kutoa elimu juu ya umuhimu wa ulipaji wa kodi/ushuru kwa wakati.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Baada ya kufanya Mapitio ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2015/2016** na na nusu mwaka wa fedha **2016/2017** kwa muhtasari naomba sasa niwasilishe makisio ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha **2017/2018**.

## 3.0 MAKISIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Ndugu Mwenyekiti,**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2017/2018**, Halmashauri inaomba kuidhinishwa jumla ya **Tsh. 33,064,812,501.00** ikiwa ni ongezeko la **1.19%** ya bajeti ya **Tsh. 32,676,659,332.02** kwa mwaka wa fedha **2016/2017**.

Mchanganuo wa bajeti kwa mwaka wa fedha **2017/2018** ni kama ifuatavyo:-

**Mchanganuo wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018**

| NA | MAELEZO | MAKISIO MWAKA 2017/2018 |
|---|---|---|
| 1. | Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri | 1,953,237,140.00 |
| 2. | Ruzuku ya matumizi Mengineyo | 2,267,523,000.00 |
| 3. | Mishahara | 22,097,612,000.00 |
| 4. | Miradi ya Maendeleo | 6,746,440,361.00 |
| | **JUMLA** | **33,064,812,501.00** |

**Ndugu Mwenyekiti,**

Sababu za msingi zilizosababisha ongezeko la bajeti ya mwaka wa fedha **2017/2018** ukilinganisha na mwaka wa fedha **2016/2017** ni kama ifuatavyo:-

i. Kupanda kwa kiwango cha makadirio ya mapato ya ndani kutoka **Tsh. 1,833,390,000.00** kwa mwaka wa fedha **2016/2017** hadi **Tsh. 1,953,237,140.00** kwa mwaka wa fedha **2017/2018.**

ii. Ongezeko la bajeti ya mishahara kutokana na mabadiliko ya viwango vya mishahara kwa watumishi waliopo na idadi ya watumishi wa nafasi wazi kwa mwaka wa fedha **2017/2018** ambapo bajeti imeongezeka kutoka Tsh. **17,733,133,000.00** kwa mwaka wa fedha **2016/2017** hadi Tsh. **22,097,612,000.00** kwa mwaka wa fedha **2017/2018**.

Aidha bajeti ya matumizi mengineyo imepungua kutoka **Tsh. 2,556,766,000.00** hadi **Tsh. 2,267,523,000.00** na bajeti ya Maendeleo pia imepungua kutoka **Tsh. 9,059,338,499.60** hadi **Tsh. 6,746,440,361.00.**

## 4.0 MAENEO YA KIPAUMBELE YA MIRADI YA MAENDELEO KWA KUTUMIA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI (OS)

**Ndugu Mwenyekiti,**

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inategemea kutumia **Tsh. 1,031,068,284.00** zikiwa ni asilimia **60** ya fedha za mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha **2017/2018** kwa shughuli za maendeleo kama inavyoonesha kwenye jedwali lifuatalo na kwenye MTEF (uk. 212-225):-

| NA | SHUGHULI | FEDHA ZILIZOTENGWA |
|---|---|---|
| 1. | Ufuatiliaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo | 47,999,000.00 |
| 2. | Kuchangia miradi inayotekelezwa na mitaa | 30,686,286.00 |
| 3. | Kulipia mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 120,000,000.00 |
| 4 | Ukamilishaji wa ujenzi wa ofisi za kata 4 | 50,000,000.00 |
| 5. | Kuuisha Mpango Mkakati wa Halmashauri | 21,088,200.00 |
| 6. | Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa shule za msingi | 215,000,000.00 |
| 7. | Ukamilishaji wa maabara shule za sekondari | 90,000,000.00 |
| 8. | Kupima maeneo ya Taasisi za Umma | 25,740,000.00 |
| 9. | Kulipia fidia ya viwanja | 47,724,798.00 |
| 10. | Kuongeza miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya | 105,000,000.00 |
| 11. | Matengezo ya barabara | 30,000,000.00 |
| 12. | Kuchangia mifuko ya maendeleo ya wanawake na vijana | 168,330,000.00 |
| 13. | Kuchangia shughuli za kilimo | 20,000,000.00 |
| 14. | Kuchangia shughuli za mifugo na uvuvi | 49,500,000.00 |
| 15, | Ujenzi wa ghuba la kukusanyia taka | 10,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **1,031,068,284.00** |

## 5.0 MALENGO MAKUU YA MPANGO (VIPAUMBELE)

**Ndugu Mwenyekiti,**

Malengo makuu ya mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha **2017/2018** ni kama ifuatavyo:-

| NA | KIPAUMBELE | FEDHA ZILIZOTENGWA |
|---|---|---|
| 1. | Kuongeza miundombinu ya shule za Msingi na Sekondari | 552,767,000.00 |
| 2. | Kuongeza miundombinu ya kutolea huduma za afya | 169,000,000.00 |
| 3. | Kuboresha barabara na miundombinu yake | 5,643,989,361.00 |
| | **JUMLA** | **6,365,756,361.00** |

## 6.0 WACHANGIAJI WENGINE WA MAENDELEO

**Ndugu Mwenyekiti,**

Katika Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri inaye mchangiaji mkubwa wa maendeleo ambaye ni Benki ya Dunia kupitia programu ya kuboresha miji (ULGSP) ambayo inaboresha miundombinu ya barabara, mazingira na kujenga uwezo wa taasisi katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Naomba sasa kuwasilisha ombi la **Tsh. 33,064,812,501.00** kwa ajili ya kutekeleza Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha **2017/2018** ikiwa inajumuisha bajeti ya Mapato ya Ndani, Matumizi mengineyo, Mishahara na Miradi ya Maendeleo.

Naomba kuwasilisha.

Fidelica G. Myovella
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA**
**MUSOMA**